GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6708 **27 Juni, 2018** **Bei Shs. 3,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo 42

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. : Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, 2018

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Mei, 2018 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
10 Aprili, 2018

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
WA
SHERIA YA KUWEKA MASHARTI BORA YA USIMAMIZI WA MAHAKAMA, KUFAFANUA UTUMISHI WA MAHAKAMA, KUANZISHA OFISI ZA MTENDAJI MKUU WA MAHAKAMA NA MRAJIS, KUANZISHA MFUKO WA MAHAKAMA, NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

UMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, 2018 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Tume;

"Jaji Mkuu" itakuwa na maana kama ilivyoelezwa katika Katiba;

"Tume" maana yake ni Tume ya Utumishi wa Mahakama iiyoanzishwa katika Katiba;

"Kamishna" maana yake ni mjumbe wa Tume;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Maadili ya Majaji na Mahakimu au Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama wa ngazi yoyote iliyoanzishwa chini ya Sheria hii au Kamati nyengine yoyote ambayo inaweza kuanzishwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama au Jaji Mkuu;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Mtendaji Mkuu wa Mahakama" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mahakama aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 7;

"Jaji Dhamana" maana yake ni Jaji Dhamana wa Mahakama Kuu au Divisheni ya Mahakama Kuu;

"Afisa wa Mahakama" maana yake ni mtu aliyepo katika utumishi wa Mahakama, aliyeteuliwa kutekeleza kazi na kutekeleza mamlaka ya utoaji wa uamuzi katika Mahakama za Sheria ikijumuisha Mahakama ya Kadhi;

"Muundo wa Utumishi wa Mahakama" maana yake ni muundo wa utendaji unaoelezea mpango rasmi au utaratibu wa utekelezaji wa mambo kwa madhumuni ya kuwawezesha majaji, mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama kuhudumu katika njia bora na ya uwajibikaji;

"Utumishi wa Mahakama" maana yake ni Utumishi wa Mahakama ulioanzishwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya Katiba, na Mahakama nyengine yoyote inayoweza kuanzishwa chini ya sheria yoyote;

"Mtumishi Mwengine wa Mahakama" maana yake ni mtu ambaye, asiyekuwa Jaji, Hakimu au Kadhi, anatekeleza kazi na kutekeleza mamlaka katika utumishi wa Mahakama;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahakama Kuu anayeteuliwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria hii;

"Katibu" maana yake ni Katibu wa Tume aliyetajwa katika kifungu cha 11.

Viwango vya utumishi.

4. Katika kutekeleza kazi na kutekeleza majukumu yaliyotolewa na Sheria hii, Tume na Mahakama, pamoja na mambo mengine:

(a) zitatumia umahiri wa kiufundi, miundombinu na utawala kuhakikisha kwamba matakwa ya utaratibu wa kimahakama yanafuatwa;

(b) zitatoa huduma bora kama msingi mkuu na, kwa kuendeleza msingi huu, Tume na Mahakama zitatengeneza muundo wa Mahakama wa kisasa na unaoendana na wakati na mafunzo mengine kwa ajili ya aina zote za Majaji, Mahakimu, Makadhi na aina zote za watumishi wengine;

(c) zitaongozwa katika shughuli zao na masharti husika ya Katiba na sheria nyengine;

(d) zitaimarisha kanuni za utumishi na maadili ya mahakama kama itakavyoelezwa na kanuni;

(e) hazitopendelea na hazitofungamana na siasa katika muelekeo na utekelezaji wake;

(f) zitaendeleza na kuimarisha uaminifu na uadilifu katika utendaji, na zitahakikisha kufikiwa kwa maadili yote muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kimahakama na kazi nyenginezo; na

(g) zitatumia na zitaendeleza maadili mengine kama yalivyoelezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma na yatakavyoelezwa na Kanuni.

SEHEMU YA PILI
UTAWALA

Utumishi wa Mahakama.

5.-(1) Utumishi wa Mahakama utajumuisha waajiriwa ambao wanagawika katika Majaji, Mahakimu, Makadhi na watumishi wengine wa Mahakama.

(2) Watumishi katika utumishi wa Mahakama, katika utekelezaji wa kazi zao za utoaji haki, hawatapokea maelekezo kutoka mamlaka yoyote nje ya utumishi wa Mahakama.

Muundo wa utumishi wa Mahakama.

6.-(1) Tume:

(a) itatengeneza muundo wa utumishi wa Mahakama kwa ajili ya kuwa na muundo utakaofikia malengo ya utoaji bora wa huduma;

(b) itaweka masharti katika muundo wa utumishi kama itakavyoona ni muhimu kwa ajili ya ukuzaji, uendelezaji, utunzaji na udhibiti wa utumishi wenye ufanisi;

(c) itatengeneza muundo wa utumishi kwa madhumuni ya ufafanuzi unaofaa na ugawaji wa majukumu yanayofanywa na Mahakama.

(2) Tume, baada ya kutengeneza muundo wa utumishi, itaupendekeza muundo huo kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

(3) Tume, katika kuteua Mahakimu, Makadhi na watumishi wengine, itazingatia vigezo na masharti yaliyowekwa katika muundo wa utumishi wa Mahakama.

Uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

7.-(1) Kutakuwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, ambaye, kwa mapendekezo ya Tume, atateuliwa na Rais.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Tume itapendekeza kwa Rais si chini ya majina matatu ambapo kutoka katika majina hayo Rais atateua Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

(3) Mtu atafaa kuteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ikiwa mtu huyo:

(a) awe mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika utawala wa umma, sheria, fedha, usimamizi wa biashara au fani nyengine zinazofanana na hizo;

(c) awe na uzoefu wa angalau miaka saba katika Utumishi wa Umma; na

(d) ni muadilifu na ana tabia njema.

(4) Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakuwa ni mkuu wa utawala wa Mahakama.

(5) Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakuwa:

(a) Afisa Mtendaji Mkuu wa Mahakama; na

(b) anawajibika kwa Jaji Mkuu kwa shughuli za kila siku za utawala katika utumishi wa Mahakama.

(6) Mtendaji Mkuu wa Mahakama atashika wadhifa huo kwa mujibu wa utaratibu na masharti kama Rais atakavyoamua.

Kazi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

8.-(1) Kazi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama zitakuwa ni:

(a) kutekeleza shughuli za jumla za utawala katika utumishi wa Mahakama pamoja na mipango, rasilimali watu, uendeshaji na utawala;

(b) kutayarisha na kuwasilisha ripoti za robo mwaka kuhusu utawala katika utumishi wa Mahakama;

(c) kutekeleza maamuzi ya Tume; na

(d) kutekeleza kazi na kutekeleza mamlaka mengine aliyopewa au anayoweza kupewa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, mamlaka ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama hayatajumuisha jambo lolote walilopewa kwa mujibu wa sheria Majaji, Mahakimu na Makadhi.

Utekelezaji wa kazi na mamlaka ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

9.-(1) Pale Mtendaji Mkuu wa Mahakama hatakuwepo kwa dharura ya muda mfupi, au Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama iko wazi, au Mtendaji Mkuu wa Mahakama anashindwa kutekeleza kazi au mamlaka yake, Jaji Mkuu:

(a) ikiwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama hayupo kwa dharura ya muda mfupi usiozidi mwezi mmoja, atateua mtu yeyote, kutoka miongoni mwa waajiriwa waandamizi katika Utumishi wa Mahakama kutekeleza kazi na kutekeleza majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama, na ataitaarifu Tume ipasavyo;

(b) ikiwa ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama iko wazi, atalipeleka suala hilo kwenye Tume kwa ajili ya uteuzi wa mtu atakayekaimu nafasi hiyo, na atamtaarifu Rais ipasavyo; au

(c) ikiwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama anashindwa kutekeleza majukumu yake au kutekeleza mamlaka yake kwa zaidi ya mwaka mmoja, atamtaarifu Rais ipasavyo.

(2) Mtu anayeteuliwa kukaimu katika nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakuwa na sifa zile zile zilizotajwa katika kifungu cha 7(3).

Mtendaji wa Mahakama Msaidizi.

10.-(1) Tume inaweza kuteua katika kila Mkoa Mtendaji wa Mahakama Msaidizi ambae vigezo na masharti yake ya utumishi yataelezwa katika barua yake ya uteuzi.

(2) Mtendaji wa Mahakama Msaidizi atakuwa na sifa zinazofanana na zile zinazohitajika kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

(3) Mtendaji wa Mahakama Msaidizi atatekeleza kazi na atatimiza majukumu kama atakavyoelekezwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu cha 9, Mtendaji wa Mahakama Msaidizi atatekeleza majukumu ya kila siku ya kiutawala ya utumishi wa Mahakama katika Mahakama ambayo Mtendaji wa Mahakama Msaidizi anapangiwa, na:

(a) atatayarisha na kuwasilisha kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ripoti za robo mwaka kuhusu utawala katika utumishi wa Mahakama;

(b) atamshauri Mtendaji Mkuu wa Mahakama katika mambo yanayohusu fedha, ununuzi na mambo mengine yasiyokuwa ya utoaji wa maamuzi ya kimahakama; na

(c) kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mahakama ambayo Mtendaji wa Mahakama Msaidizi huyo anapangiwa.

(5) Katika utekelezaji wa majukumu yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (3), Mtendaji wa Mahakama Msaidizi atawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Jaji Dhamana au Hakimu Dhamana, kama hali itakavyokuwa.

Tume ya Utumishi wa Mahakama.

11.-(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama kama ilivyoanzishwa na Katiba.

(2) Muundo wa Tume ya Utumishi wa Mahakama utakuwa kama ulivyoelezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama atawajibika kuhakikisha na kuwezesha utekelezaji wa maamuzi ya Tume.

(4) Mjumbe wa Tume hatawakilishwa katika mkutano na mwakilishi na mjumbe hatakasimu kwa mtu yeyote utekelezaji wa kazi yoyote au utekelezaji wa jukumu ambalo kikawaida linatekelezwa na yeye mwenyewe au wajibu ambao kikawaida unafanywa na yeye mwenyewe kwa nafasi yake ya kuwa mjumbe wa Tume.

(5) Uendeshaji wa mikutano na utaratibu wa kufanya maamuzi ya Tume utakuwa kama ulivyoelezwa katika Jadweli ya Kwanza ya Sheria hii.

(6) Tume ya Utumishi wa Mahakama, katika utekelezaji wa kazi zake, itakuwa inashauriana mara kwa mara na Jaji Mkuu.

Uwezo wa Tume.

12.-(1) Tume, pamoja na uwezo iliyopewa na Sheria ya Utumishi wa Umma, itakuwa na uwezo na itatekeleza mamlaka kuhusiana na uteuzi, uthibitishaji, upandishaji wa vyeo na nidhamu.

(2) Tume, kwa madhumuni ya uajiri, uthibitishaji, upandishaji wa vyeo na nidhamu, itaanzisha Kamati ya Ushauri ya Ajira.

(3) Tume itaamua juu ya muundo na taratibu za Kamati ya Ushauri ya Ajira na itaweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake.

(4) Jaji, Hakimu, Kadhi au mtumishi mwengine wa Mahakama asiyekuwa Jaji, Hakimu au Kadhi ambaye hajaridhika na uamuzi wa Tume kuhusiana na utekelezaji wa mamlaka yake anaweza kukata rufaa kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Kazi za Tume.

13.-(1) Kazi za Tume zitakuwa:

(a) kupendekeza kwa Rais kuhusiana na:

(i) uteuzi wa Majaji;

(ii) uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis;

(iii) kumsimamisha kazi Jaji;

(b) kupeleka taarifa kwa Rais kuhusiana na tabia mbaya ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama au Mrajis ambayo inakwenda kinyume na maadili ya ofisi zao au inayokwenda kinyume na sheria zinazoongoza maadili ya viongozi wa umma;

(c) kupendekeza kwa Jaji Mkuu kuhusiana na kutokuweza kwa Jaji kutekeleza kazi za ofisi; au kupeleka taarifa kwa Jaji Mkuu kuhusiana na tabia mbaya ya Jaji;

(d) kuchunguza malalamiko dhidi ya Jaji, Hakimu, Kadhi au mtumishi mwengine asiyekuwa Jaji, Hakimu au Kadhi;

(e) kuchukua hatua za kiutawala na za kinidhamu dhidi ya Jaji isipokuwa zile zilizotajwa katika Katiba;

(f) kuteua Mrajis wa Mahakama ya Kadhi na Mahakimu, Makadhi isipokuwa Jaji Mkuu, Jaji, Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu na Kadhi wa Rufaa;

(g) kupandisha cheo Hakimu au Kadhi yeyote;

(h) kuchukua hatua za kinidhamu kwa Hakimu au Kadhi; na

(i) kuajiri, kuthibitisha ajira, kupandisha cheo na kuchukua hatua za kinidhamu au hatua za kiutawala dhidi ya mtumishi wa Mahakama asiyekuwa Jaji, Hakimu au Kadhi.

(2) Tume itashauri na kupendekeza Serikalini mishahara na stahiki za Majaji, Mahakimu, Makadhi na maafisa wa Mahakama wasiokuwa Majaji, Mahakimu au Makadhi katika utumishi wa Mahakama.

Mapitio ya Maslahi.

14. Endapo inaona ni vyema na ni muhimu kupitia mishahara, marupurupu, maslahi na vigezo na masharti ya utumishi wa waajiriwa wa utumishi wa Mahakama, Tume itapitia mishahara, marupurupu, maslahi, vigezo na masharti ya utumishi, na itapendekeza Serikalini.

Kukasimu kazi.

15.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Tume inaweza, kwa Kanuni, kukasimu utekelezaji wa kazi yoyote iliyopewa, isipokuwa kazi zile iliyopewa na Katiba, kwa Kamati zilizoanzishwa au ambazo zitakazoweza kuanzishwa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kukasimu kazi zake kama ifuatavyo:

(a) kupeleleza na kuchunguza malalamiko dhidi ya Majaji kwa Kamati ya Maadili ya Majaji iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;

(b) kupeleleza na kuchunguza kuhusiana na nidhamu za Mahakimu , Makadhi na watumishi wengine wa Mahakama kwa Kamati ya Maadili ya watumishi wa Mahakama iliyoanzishwa chini ya Sheria hii.

(3) Katika Kanuni zozote zilizotungwa kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume itaainisha maafisa ambao kukasimu huko kutatumika.

(4) Tume inaweza kutekeleza kazi zozote hizo zilizotajwa bila kujali kukasimu huko kwa utekelezaji huo kwa mtu mwengine.

(5) Katika utekelezaji wa shughuli zake, Tume itaongozwa na taratibu zilizoainishwa katika Jadweli ya Kwanza ya Sheria hii.

Uwezo wa kuachisha na kuondoa.

16.-(1) Uwezo wa kuwaondoa katika ofisi au kusitisha teuzi za Mahakimu, Makadhi na watumishi wasiokuwa Mahakimu au Makadhi isipokuwa Jaji Mkuu, Majaji wa Mahakama Kuu, Mrajis, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu utatekelezwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(2) Hakimu, Kadhi au mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi hataachishwa kazi isipokuwa kama Tume itaridhika kwamba:

(a) kosa la kinidhamu limefanywa na limethibitishwa kwa mizania ya uwezekano dhidi ya Hakimu, Kadhi au mtumishi huyo kutokana na sababu zote au sababu yoyote miongoni mwa zifuatazo:

(i) tabia mbaya isiyolingana na nafasi ya Hakimu, Kadhi au nafasi ya mtumishi asiyekuwa hakimu au Kadhi;

(ii) uzembe mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Hakimu au Kadhi au majukumu yasiyokuwa ya Hakimu au Kadhi;

(iii) kuvunja kanuni za maadili; au

(iv) sifa mbaya isiyolingana na nafasi ya Hakimu au Kadhi au nafasi ya mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi;

(b) Hakimu, Kadhi au mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi huyo alipewa fursa ya kujibu shtaka chini ya aya ya (a); na

(c) uchunguzi umefanywa kuhusu kosa hilo.

Viapo.

17.-(1) Mwenyekiti, Wajumbe wa Tume na Katibu wa Tume, katika uteuzi, watakula kiapo au watathibitisha katika fomu iliyowekwa katika Jadweli ya Pili ya Sheria hii.

(2) Mwenyekiti wa Tume anaweza kumtaka mjumbe wa Sekretarieti ya Tume, katika uteuzi wa mwanzo, kula kiapo au kuthibitisha katika fomu iliyowekwa katika Jadweli ya Pili ya Sheria hii.

(3) Endapo Mwenyekiti, mjumbe yeyote wa Tume au Sekretarieti ya Tume ametakiwa kula kiapo au]' kuthibitisha chini ya kifungu hiki hana imani ya dini, au ulaji kiapo huo au uthibitisho huo ni kinyume na imani ya dini yake, anaweza kula kiapo kwa kuthibitisha katika fomu ya kiapo au fomu ya uthibitisho iliyowekwa, atabadilisha maneno "kwa dhati na kwa uaminifu nakiri na kuthibitisha" badala ya neno "naapa" na kuondoa maneno "Ewe Mungu nisaidie".

(4) Kiapo au uthibitisho unaofanywa na Mwenyekiti wa Tume au mjumbe wa Tume utasimamiwa na Jaji Mkuu na kila kiapo au uthibitisho unaofanywa na Katibu au mjumbe wa Sekretarieti utasimamiwa na Mwenyekiti wa Tume.

Nafasi wazi katika wajumbe na maamuzi.

18.-(1) Kwa mujibu wa utaratibu wa kanuni za Tume, uamuzi na hatua za Tume hazitakuwa batili kwa sababu tu ya kuwa wazi kwa nafasi ya ujumbe au ya kutokuwepo kwa mjumbe yeyote.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), uamuzi wa Tume utatakiwa kuungwa mkono na wajumbe walio wengi waliohudhuria.

Utaratibu.

19. Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, au kwa Kanuni yoyote iliyowekwa na Jaji Mkuu, Tume itasimamia yenyewe taratibu zake.

Kinga.

20. Mjumbe wa Tume, katika hali ya hatua yoyote au kesi iliyoletwa dhidi ya mjumbe huyo kwa kitendo kilichotendwa au kuacha kutendwa kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu, atakuwa na kinga ile ile na fursa kama ile iliyowekwa na Sheria kwa vitendo vilivyotendwa au kwa maneno yaliyotamkwa na Jaji wa Mahakama Kuu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kimahakama.

Mawasiliano ya Tume kuwa na kinga.

21. Mtu, katika mwenendo wowote wa kisheria, hataruhusiwa au kulazimishwa kutoa au kuweka bayana mawasiliano yoyote, ikiwa kwa njia ya maandishi au kwa njia ya mdomo, ambayo yamefanywa:

(a) baina ya Tume, au mjumbe yeyote, au afisa wa Tume, au Kamisheni ya Utumishi wa Umma, au mjumbe yeyote ama wa Tume au wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma;

(b) baina ya mjumbe yeyote au afisa wa Tume na Mwenyekiti wa Tume hiyo; au

(c) baina ya mjumbe yeyote au maafisa wa Tume, katika utekelezaji wa, au kuhusiana na utekelezaji wa, majukumu na kazi za Tume,

isipokuwa kama Mwenyekiti wa Tume anaridhia kwa maandishi utoaji au uwekaji bayana huo wa mawasiliano.

SEHEMU YA TATU
JAJI MKUU NA MRAJIS

Jaji Mkuu na Kamati ya Uongozi.

22.-(1) Jaji Mkuu atakuwa Mkuu wa Mahakama, na, pamoja na kazi zilizoelezwa katika Katiba au sheria nyengine yoyote, atatekeleza kazi na mamlaka yaliyoelezwa katika Sheria hii.

(2) Kutakuwa na Kamati ya Uongozi ya Mahakama ambayo wajumbe wake watakuwa ni Jaji Mkuu na wajumbe wengine watakaoteuliwa na Jaji Mkuu.

(3) Jaji Mkuu atakuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi.

(4) Kamati ya Uongozi:

(a) itamshauri Jaji Mkuu katika mambo ya jumla yanayohusu uendeshaji wa Mahakama;

(b) itamshauri Jaji Mkuu kuhusiana na makadirio ya bajeti ya Mahakama; na

(c) itamshauri Jaji Mkuu kwa jambo lolote ambalo anaweza kuhitaji ushauri.

(5) Jaji Mkuu ataitisha vikao vya Kamati ya Uongozi.

(6) Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Uongozi.

Uwezo wa Jaji Mkuu.

23.-(1) Jaji Mkuu, kwa madhumuni ya upatikanaji wa utekelezaji bora, utekelezaji mzuri na utekelezaji wenye ufanisi wa kazi za ofisi za majaji wa Mahakama Kuu na mahakimu, atasimamia umalizaji na uendeshaji wa kesi.

(2) Katika kutekeleza mamlaka ya usimamizi, Jaji Mkuu anaweza:

(a) kumtaka Jaji au Hakimu yeyote isipokuwa Kadhi kuwasilisha taarifa za umalizikaji wa kesi ndani ya kipindi kilichoainishwa;

(b) kupokea na kupeleleza malalamiko yoyote yanayohusiana na umalizikaji wa kesi yoyote;

(c) kuchukua hatua zozote kama itakavyokuwa inafaa kushughulikia jambo lolote ambalo ni kiini cha lalamiko;

(d) kuitisha mkutano wa usimamizi wa kesi; au

(e) kulipeleka jambo lolote ambalo ni kiini cha malalamiko kwa Tume.

(3) Jaji Mkuu anaweza, kuhusiana na usimamizi wa Mahakama, kukasimu lolote katika mamlaka yake na kazi chini ya kifungu hiki kwa Majaji Dhamana.

Wajibu wa Jaji Mkuu.

24.-(1) Jaji Mkuu atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi za Mahakama, zikiwemo utoaji wa maelekezo, usimamizi wa vikao vya Mahakama na ugawaji wa majukumu ya Mahakama.

(2) Maelekezo ya majukumu yatajumuisha, bila ya kuzuia ujumla wa masharti hayo, uwezo wa:

(a) kuamua vikao vya Mahakama;

(b) kupanga majaji wa vikao;

(c) kupanga kesi na majukumu mengine ya kimahakama kwa majaji;

(d) kuamua ratiba za vikao na pahala pa vikao kwa majaji;

(e) kuamua idadi ya wingi wa kazi za majaji kwa mwaka, mwezi na wiki; na

(f) kuandaa orodha ya usikilizaji wa kesi na kupanga vyumba vya Mahakama.

(3) Watendaji wengine wa Mahakama wasiokuwa Majaji, Mahakimu na Makadhi watafanya kazi kwa maelekezo ya Jaji Mkuu katika mambo ambayo yamewekwa na Sheria kwa Mahakama.

(4) Watu waliotajwa katika kifungu kidogo cha (3) ambao wamepewa majukumu katika vyumba vya Mahakama, kwa maelekezo ya Jaji ambaye anasimamia mwenendo wa kesi katika chumba cha Mahakama, watatekeleza majukumu hayo.

Mrajis.

25.-(1) Kutakuwa na Mrajis wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Rais baada ya mapendekezo ya Tume.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Tume itapendekeza kwa Rais si chini ya majina matatu ambapo kutoka katika majina hayo Rais atateua Mrajis wa Mahakama Kuu.

(3) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kama Mrajis ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya sheria;

(c) ameshafanya kazi katika fani ya sheria kwa kipindi kisichopungua miaka saba; na

(d) mwenye maadili na tabia njema.

(4) Mrajis atasaidiwa na Naibu Warajis watakaoteuliwa na Tume.

(5) Naibu Warajis watakuwa na sifa sawa na zile zinazohitajika kwa Mrajis.

(6) Mrajis atawajibika kwa Jaji Mkuu kwa utekelezaji bora wa kazi za Mahakama.

Kazi za Mrajis.

26.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya vifungu vidogo vya (4) na (5) vya kifungu cha 25, Mrajis:

(a) atawezesha na kusimamia utekelezaji wa kazi za Mahakama;

(b) ataratibu shughuli za Mahakama;

(c) ataoanisha, atatengeneza na atatoa taarifa ya jumla ya utekelezaji wa kazi za Mahakama;

(d) ataweka kiunganishi baina ya Mahakama na Tume katika uteuzi, upandishaji vyeo na mambo ya kinidhamu ya Majaji, Mahakimu na Makadhi;

(e) atawasiliana na Serikali kuhusiana na mambo yanayohusu taaluma ya Mahakama, au mambo mengine yoyote ambayo Serikali inaweza kuhusika.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Naibu Warajis watawajibika kwa Mrajis na kwa msingi huo, watatekeleza kazi na majukumu kama watakavyoweza kupangiwa na Mrajis.

(3) Mrajis:

(a) ataandaa kalenda ya mwaka ya Mahakama;

(b) atatekeleza majukumu hayo kama yalivyoelezwa katika sheria yoyote au Kanuni za Mahakama;

(c) ataandaa amri na dikirii ya Mahakama kama itakavyoelekezwa na Mahakama;

(d) atatekeleza au atahakikisha utekelezwaji wa amri za Mahakama;

(e) atakuwa, na atatekeleza majukumu ya mtozaji ushuru wa Mahakama;

(f) atasimamia majukumu yanayohusiana na Mahakama kama yatakavyokasimiwa kwa Naibu Warajis; na

(g) atatekeleza kazi nyengine zilizoelezwa na sheria nyengine yoyote.

SEHEMU YA NNE
UANZISHAJI WA KAMATI ZA MAADILI

Kamati za Maadili.

27. Tume ya Utumishi wa Mahakama itakuwa na Kamati za Maadili za ngazi mbili tofauti ambazo zitakuwa na wajibu wa kufanya upelelezi na uchunguzi dhidi ya Majaji, Mahakimu, Makadhi na watumishi wasiokuwa Majaji, Mahakimu au Makadhi.

(a) Kamati ya Maadili ya Majaji

Uanzishaji na muundo wa Kamati ya Maadili ya Majaji.

28.-(1) Tume inaweza, pale itakapohitajika, kuunda Kamati ya Maadili ya Majaji ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Jaji Mwandamizi wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Tume kwa kushauriana na Jaji Mkuu – Mwenyekiti;

(b) Jaji wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Tume - Mjumbe;

(c) mtu mwenye sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Tume - Mjumbe; na

(d) Mrajis atakuwa Katibu wa Kamati ya Maadili ya Majaji.

(2) Kamati ya Maadili ya Majaji haitokasimu kwa mtu yeyote utekelezaji wa kazi yoyote au utekelezaji wa mamlaka yoyote.

(3) Jaji hatokuwa Mwenyekiti wala Mjumbe wa Kamati ya Maadili ya Majaji ikiwa lalamiko linalopelelezwa au kuchunguzwa linamhusu Jaji huyo.

Kazi za Kamati ya Maadili ya Majaji.

29.-(1) Kazi za Kamati ya Maadili ya Majaji zitakuwa ni:

(a) kupokea na kupeleleza malalamiko dhidi ya Jaji;

(b) kumpelekea Jaji husika malalamiko hayo;

(c) kusikiliza malalamiko;

(d) kupendekeza kwenye Tume hatua za kuchukuliwa dhidi ya Jaji, kuhusiana na malalamiko yoyote inayoyaona siyo makubwa; na

(e) kuchukua hatua nyengine zozote kama itakavyoona ni muhimu katika mazingira husika.

(2) Malalamiko dhidi ya Jaji ambayo Kamati ya Maadili ya Majaji inayoyaona kuwa ni makubwa yatawasilishwa katika Tume na kwa Jaji Mkuu kwa mazingatio.

(3) Katika utekelezaji wa shughuli zake, Kamati ya Maadili ya Majaji itaongozwa na utaratibu ulioainishwa katika Jadweli ya Tatu.

Malalamiko mbele ya Kamati ya Maadili ya Majaji.

30.-(1) Malalamiko dhidi ya Jaji yanaweza kutolewa na:

(a) yeyote miongoni mwa walalamikaji wafuatao:

(i) Jaji, Hakimu au Kadhi;

(ii) mtumishi asiyekuwa Jaji, Hakimu au Kadhi;

(iii) taasisi ya Serikali;

(iv) wakili au vakili;

(v) mtu mwenye maslahi katika jambo husika; au

(b) katika mazingira mengine yoyote, mtu ambaye anayeweza kuleta ushahidi wa kutosha juu ya malalamiko hayo.

(2) Malalamiko dhidi ya Jaji yatapelekwa kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye atayapeleka malalamiko hayo kwenye Tume na Tume itayashughulikia malalamiko hayo kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria hii.

Muundo na maudhui ya malalamiko.

31.-(1) Malalamiko yatatolewa kwa maandishi na yatasainiwa na mlalamikaji.

(2) Malalamiko yatajumuisha taarifa za kutosha zinazoweka wazi kutenda au kuacha kutenda kunakolalamikiwa na mazingira ambayo kutenda huko au kuacha kutenda huko kumetokea.

(3) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (2), malalamiko yanaweza kutolewa kuhusu jambo lolote miongoni mwa mambo yafuatayo:

(a) ushughulikiaji wa kesi;

(b) tuhuma ya rushwa;

(c) tabia isiyoendana na Kanuni za Maadili ya Mahakama; au

(d) kushindwa kutekeleza kazi za Jaji.

(4) Malalamiko hayatokataliwa kwa sababu tu yana kasoro katika muundo.

Utaratibu wa Tume kushughulikia malalamiko.

32. Tume inaweza, baada ya kupokea lalamiko na pale inapoona inafaa kufanya hivyo:

(a) itaunda Kamati ya Maadili ya Majaji na italipeleka lalamiko dhidi ya Jaji kwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo;

(b) kumpelekea lalamiko hilo Jaji husika anayelalamikiwa na kumtaka ajibu ndani ya kipindi kisichozidi siku ishirini na moja; au

(c) katika jambo ambalo ni dogo na halistahili kupelekwa kwa Jaji Mkuu, kuchukua hatua ambazo ni muhimu kulishughulikia lalamiko hilo.

Kamati ya Maadili ya Majaji kushughulikia lalamiko.

33. Kamati ya Maadili ya Majaji inaweza, baada ya kupokea lalamiko lolote kutoka kwenye Tume, endapo:

(a) inaona inafaa, itawasilisha lalamiko hilo kwa Jaji husika anayelalamikiwa na kumtaka ajibu ndani ya kipindi kisichozidi siku ishirini na moja; na

(b) itaona ni vyema, itawezesha kufanywa upelelezi kuhusu lalamiko hilo na itachunguza kuhusu jambo hilo.

Utaratibu pale Jaji hakubali lalamiko.

34. Endapo jambo lipo mbele ya Kamati ya Maadili ya Majaji na Jaji husika anayelalamikiwa hakubali lalamiko hilo, na baada ya uchunguzi, Kamati ya Maadili ya Majaji inaona lalamiko hilo ni kubwa, itapeleka taarifa ya uchunguzi wa jambo hilo katika Tume na kwa Jaji Mkuu.

(b) Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama

Uanzishaji na muundo wa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama.

35.-(1) Inaanzishwa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama kwa ajili ya Mahakimu na watumishi wasiokuwa mahakimu, ambao wasiokuwa Majaji wa Mahakama Kuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu, na itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Jaji Mwandamizi wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Tume kwa kushauriana na Jaji Mkuu – Mwenyekiti;

(b) Hakimu Mwandamizi mmoja atakayeteuliwa na Tume - Mjumbe;

(c) Kadhi mmoja atakayeteuliwa na Tume - Mjumbe; na

(d) watumishi wawili wasiokuwa Mahakimu au Makadhi watakaoteuliwa na Tume - Wajumbe.

(2) Naibu Mrajis atakayeteuliwa na Tume, atakuwa Katibu wa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama.

(3) Wajumbe wa Kamati watashikilia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini wataweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(4) Kamati haitakasimu kwa mtu yeyote utekelezaji wa kazi au utekelezaji wa mamlaka yoyote.

(5) Naibu Mrajis ambaye dhidi yake lalamiko limetolewa, hatakuwa Katibu wa Kamati ambayo inaamua lalamiko hilo.

(6) Hakimu au Kadhi na mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi ambaye dhidi yake lalamiko limewasilishwa, hatakuwa mjumbe wa Kamati ambayo inaamua lalamiko hilo.

Kazi za Kamati ya Maadili ya Watumishi Mahakama.

36.-(1) Kazi za Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama zitakuwa ni:

(a) kupokea malalamiko dhidi ya Mahakimu na watumishi wasiokuwa Mahakimu ambao sio Majaji wa Mahakama Kuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu;

(b) kupokea lalamiko kutoka Tume;

(c) kumpelekea lalamiko hilo Hakimu, Kadhi au mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi;

(d) kuchunguza lalamiko; na

(e) kupeleka ripoti ya uchunguzi wa lalamiko kwa Tume na kwa Jaji Mkuu.

(2) Katika utekelezaji wa shughuli zake, Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama itaongozwa na utaratibu ulioainishwa katika Jadweli ya Tatu ya Sheria hii.

Malalamiko mbele ya Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama.

37.-(1) Lalamiko dhidi ya Hakimu, Kadhi au mtumishi asiyekuwa Hakimu au Kadhi linaweza kutolewa na:

(a) Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama yenyewe;

(b) yeyote miongoni mwa walalamikaji walioainishwa katika kifungu cha 30; au

(c) linaweza kuletwa mbele ya Kamati na Tume.

(2) Lalamiko dhidi ya Hakimu, Kadhi au mtumishi mwengine wa Mahakama litawasilishwa kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye anaweza kuchukua hatua za kinidhamu kwa mambo yaliyo chini ya mamlaka yake au kulipeleka lalamiko hilo katika Tume na kumuarifu Jaji Mkuu.

Utaratibu.

38. Masharti ya vifungu vya 31, 32, 33 na 34 vinavyohusiana na utaratibu wa malalamiko kama hali itakavyokuwa vitatumika katika malalamiko dhidi ya Mahakimu, Makadhi na watumishi wasiokuwa Mahakimu au Makadhi katika Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

Uanzishaji wa Mfuko wa Mahakama.

39.-(1) Unaanzishwa kwa ajili ya Mahakama, mfuko maalum utakaojulikana kama Mfuko wa Mahakama.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, viwango vya fedha vilivyoidhinishwa kwa ajili ya Mahakama vitalipwa na hazina katika Mfuko wa Mahakama.

(3) Usimamizi wa jumla na udhibiti wa Mfuko wa Mahakama utakuwa chini ya Afisa Masuuli atakayeteuliwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Misaada.

40.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 39, Mahakama inaweza kupokea kwa ajili ya na kwa niaba ya Mahakama, msaada halali wowote uliotolewa kwa ajili ya Mahakama.

(2) Viwango vyovyote vitakavyopokelewa kama msaada uliotolewa kwa Mahakama kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), vitafuata matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma.

Bajeti ya Mahakama.

41.-(1) Kabla ya kila mwaka wa fedha, Jaji Mkuu atamuelekeza Afisa Masuuli kuandaa makadirio ya kiwango cha fedha ambacho Mahakama itakihitaji kwa ajili ya malipo ya gharama mbali mbali na matumizi yatakayofanywa na Mahakama, ndani ya mwaka wa fedha kwa madhumuni yafuatayo:

(a) huduma za utawala na huduma za uwezeshaji zinazotolewa kwa Mahakama;

(b) mahitaji ya fedha kwa ajili ya kazi za Mahakama.

(2) Katika utayarishaji wa makadirio Afisa Masuuli atazingatia yafuatayo:

(a) uhalisia, kiwango na ubora wa huduma za utawala na huduma za uwezeshaji zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Mahakama;

(b) uhalisia, kiwango na ubora wa huduma za utawala na huduma za uwezeshaji ambazo Mahakama inazihitaji kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi yake ya Kikatiba; na

(c) mahitaji ya uwajibikaji wa kifedha.

(3) Afisa Masuuli atatayarisha makadirio kwa ajili ya Mahakama ndani ya mahitaji ya fedha kwa Mahakama kwa mwaka wa fedha husika.

Majadiliano ya makadirio ya bajeti na uwasilishaji.

42.-(1) Afisa Masuuli atawasilisha Hazina makadirio ya bajeti kama yalivyoridhiwa na Kamati ya Uongozi kwa ajili ya majadiliano.

(2) Baada ya kukamilika kwa majadiliano chini ya kifungu kidogo cha (1), Afisa Masuuli atawasilisha makadirio ya bajeti yaliyokubaliwa na Hazina kwa Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Sheria kwa madhumuni ya kuomba idhini ya Baraza la Wawakilishi.

Hesabu na Ukaguzi.

43.-(1) Afisa Masuuli atawezesha uwekwaji wa vitabu sahihi vya hesabu na, ndani ya na si zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa fedha, atawezesha kutayarishwa taarifa ya mapato na matumizi katika kipindi cha mwaka wa fedha.

(2) Hesabu zinazohusiana na uendeshaji wa Mfuko wa Mahakama katika siku ya mwisho ya mwaka wa fedha zitawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma.

Usimamizi na udhibiti wa fedha za Mahakama.

44. Kwa ajili ya usimamizi mzuri na udhibiti wa kifedha wa uendeshaji wa Mfuko wa Mahakama, Mtendaji Mkuu wa Mahakama atahakikisha kwamba, masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma yanafuatwa ipasavyo.

SEHEMU YA SITA
MAKOSA NA ADHABU

Kosa la kuishawishi au kujaribu kuishawishi Tume.

45.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya sheria nyengine yoyote, mtu yeyote ambaye isipokuwa kama yupo katika utekelezaji wa jukumu lake moja kwa moja au vyenginevyo kwa yeye mwenyewe au kwa mtu mwengine yeyote, katika namna yoyote ile, anashawishi au anajaribu kushawishi uamuzi wowote wa Tume, atakuwa ni mkosa na atakapotiwa hatiani, atapewa adhabu na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachozuia mtu yeyote kutoa cheti au ushahidi kwa muombaji yeyote au mtu aliyechaguliwa kuwania nafasi yoyote au kutoa taarifa yoyote au msaada kufuatia maombi ya Tume.

Kosa la kutoa taarifa ya uongo kwa Tume.

46. Bila ya kuathiri masharti ya sheria nyengine yoyote, mtu yeyote ambaye kuhusiana na utekelezaji wa kazi au majukumu ya Tume kwa makusudi anatoa taarifa yoyote kwa Tume ambayo anajua kuwa ni ya

uongo au haamini kuwa ni ya kweli, au taarifa ambayo anajua kuwa ni ya uongo kwa sababu ya kuondoshwa taarifa muhimu, atakuwa ni mkosa na atakapotiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili.

Tafsiri ya neno "Tume".

47. Kwa madhumuni ya kifungu cha 45 na 46 neno "Tume" linajumuisha Tume, mjumbe wa Tume, Katibu wa Tume, Kamati ya Tume, afisa wa Tume au mtu au kikundi cha watu walioteuliwa kuisaidia Tume katika utekelezaji wa kazi na majukumu yake.

Kutokuruhusiwa kutoa taarifa zilizozuiliwa.

48.-(1) Mjumbe wa Tume, au afisa wa Tume, au mtu mwengine yeyote, bila ya ruhusa ya maandishi ya Mwenyekiti wa Tume, hatachapisha au hataweka bayana kwa mtu yeyote isipokuwa kama yupo katika utekelezaji wa kazi zake, maudhui ya waraka wowote, mawasiliano au taarifa yoyote ile ambayo imekuja kwake kama taarifa katika utekelezaji wa majukumu yake kuhusiana na Tume, na mtu ambaye kwa kujua anatenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo hiki, atakuwa ni mkosa, na atakapotiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Mtu ambaye anajua taarifa yoyote ambayo kwa uelewa wake imewekwa bayana kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) na mtu huyo anachapisha au anaiwasilisha kwa mtu mwengine yeyote isipokuwa kama kwa madhumuni ya uendeshaji wa mashtaka yoyote chini ya Sheria hii au katika utekelezaji wa jukumu lake rasmi, atakuwa ni mkosa, na atakapotiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja.

Ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

49. Hakuna mashtaka kuhusiana na kosa lolote chini ya Sehemu hii yatakayoanzishwa isipokuwa kwa ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA JUMLA

Kanuni.

50.-(1) Jaji Mkuu anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya uendeshaji wa Mahakama.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), Kanuni zinaweza:

(a) kuwataka watu kufika mbele ya Tume kujibu maswali yanayohusu utekelezaji wa mamlaka ya Majaji, Mahakimu na Makadhi;

(b) kuweka masharti tofauti kwa ngazi tofauti za Majaji, Mahakimu na Makadhi; na

(c) kuelezea Kanuni za Kazi na Maadili kwa Majaji, Mahakimu na Makadhi na watendaji wengine wasiokuwa Majaji, Mahakimu au Makadhi;

(3) Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii zitachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kufuta.

51. Kifungu cha 6 cha Sheria ya Mahakama Kuu Nam. 2 ya 1985 kinafutwa.

JADWELI
JADWELI YA KWANZA
(Kifungu cha 11 na 15)

MIKUTANO NA MWENENDO WA TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

Mikutano ya Tume.

1.-(1) Tume kikawaida itakutana kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake katika muda na pahala patakapoamuliwa na Tume, lakini itakutana angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti anaweza, katika wakati wowote yeye mwenyewe au kufuatia maombi ya wajumbe walio wengi, kuitisha mkutano maalum wa Tume.

(3) Mwenyekiti ataendesha mkutano wowote wa Tume na asipokuwepo Mwenyekiti wajumbe waliohudhuria watamteua mmoja miongoni mwao kuendesha mkutano huo.

(4) Mwenyekiti anaweza kumualika mtu ambaye siyo mjumbe kushiriki katika majadiliano ya mkutano wowote wa Tume lakini mtu huyo aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi.

2. Akidi ya mkutano wa Tume itakuwa kwa wingi wa wajumbe waliokuwepo.

Uamuzi wa Tume.

3.-(1) Jambo lililowasilishwa katika Mkutano wa Tume litaamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria, na itakapotokezea kura kuwa sawa, mtu anayeendesha mkutano atakuwa na kura ya ziada pamoja na kura yake halisi au kura ya kawaida.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), uamuzi wa Tume unaweza kufanywa kwa wingi wa wajumbe bila ya mkutano kwa njia ya toleo la waraka husika miongoni mwa wajumbe, kwa kueleza kwa njia ya maandishi.

Kumbu-kumbu za mikutano.

4.-(1) Katibu atarekodi na kuweka kumbukumbu za shughuli zote zilizofanywa au zilizotekelezwa katika mikutano ya Tume na kumbukumbu za kila mkutano wa Tume zitasomwa na kuthibitishwa, au kurekebishwa na kuthibitishwa, katika mkutano mwengine ambao kumbukumbu zake zitadaiwa kuwepo.

(2) Kumbukumbu zinazodaiwa kusainiwa na mtu anayeendesha mkutano wa Tume, ikiwa hakuna uthibitisho wa kosa, zitachukuliwa kuwa ni kumbukumbu sahihi za mkutano ambao kumbukumbu zake zinadaiwa kuwepo.

5. Uhalali wa kitendo chochote au mwenendo wa Tume hautaathirika kwa kutokuwepo miongoni mwa wajumbe wake. Kutokuwepo hakutabatilisha mwenendo wa mkutano.

6. Amri, maelekezo, notisi au nyaraka nyengine zilizofanywa au kutolewa kwa niaba ya Tume zitasainiwa na: Amri na maelekezo.

(a) Mwenyekiti; au

(b) Katibu au mjumbe mwengine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kufanya hivyo kwa niaba ya Mwenyekiti.

7. Kwa kuzingatia masharti ya Jadweli hili, Tume inaweza kusimamia yenyewe mwenendo wa mikutano yake. Tume inaweza kusimamia yenyewe mwenendo wa mikutano yake.

JADWELI YA PILI
(Kifungu cha 17)

KIAPO CHA MWENYEKITI NA MJUMBE

Mimi,…….niliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti/Mjumbe/Katibu/Mjumbe wa Sekretarieti wa Tume ya Utumishi ya Mahakama ninaapa/ninathibitisha/ninatamka kwamba nitatekeleza kazi zangu za Mwenyekiti/Mjumbe/Katibu wa Tume, kwa uhuru na bila ya woga au upendeleo, utashi au nia mbaya, na kwamba sitatoa jambo lolote linalohusiana na kazi za Tume moja kwa moja au vyenginevyo kwa mtu yeyote asiyeruhusiwa au isipokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

EWE MWENYEZI MUNGU NISAIDIE

Imeapwa/Imethibitishwa/Imetamkwa mbele yangu leo tarehe…… mwezi……20…..

……..
Mwenyekiti/Mjumbe/Katibu wa Tume

JADWELI YA TATU
(Vifungu vya 29 na 36)

MIKUTANO NA MWENENDO WA KAMATI YA MAADILI YA MAJAJI NA KAMATI YA MAADILI YA WATUMISHI WA MAHAKAMA

Mikutano ya Kamati.

1.-(1) Kamati kikawaida itakutana kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake katika muda na pahala patakapoamuliwa na Kamati.

(2) Mwenyekiti anaweza, katika wakati wowote yeye mwenyewe au kufuatia maombi ya wajumbe walio wengi, kuitisha mkutano maalum wa Kamati.

(3) Mwenyekiti ataendesha mkutano wowote wa Kamati na asipokuwepo Mwenyekiti wajumbe waliohudhuria watamteua mmoja miongoni mwao kuendesha mkutano huo.

(4) Kamati inaweza kumualika mtu ambaye siyo mjumbe kushiriki katika majadiliano ya mkutano wowote wa Kamati lakini mtu huyo aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi.

2. Akidi ya mkutano wa Tume itakuwa kwa nusu ya wajumbe waliokuwepo.

Uamuzi wa Kamati

3. Jambo lililowasilishwa katika Mkutano wa Kamati litaamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria, na itakapotokezea kura kuwa sawa, mtu anayeendesha mkutano atakuwa na kura ya ziada pamoja na kura yake halisi au kura ya kawaida.

Kumbukumbu za mikutano.

4.-(1) Kamati itawezesha kurekodiwa na kuweka kumbukumbu za shughuli zote zilizofanywa au zilizotekelezwa katika mikutano ya Kamati na kumbukumbu za kila mkutano wa Kamati zitasomwa na kuthibitishwa, au kurekebishwa na kuthibitishwa, katika mkutano mwengine ambao kumbukumbu zake zitadaiwa kuwepo.

(2) Kumbukumbu zinazodaiwa kusainiwa na mtu anayeendesha mkutano wa Kamati, ikiwa hakuna uthibitisho wa kosa, zitachukuliwa kuwa ni kumbukumbu sahihi za mkutano ambao kumbukumbu zake zinadaiwa kuwepo.

Kutokuwepo hakutabatilisha mwenendo wa mkutano.

5. Uhalali wa kitendo chochote au mwenendo wa Kamati hautaathirika kwa kutokuwepo miongoni mwa wajumbe wake au kwa kasoro yoyote inayotokana na uteuzi wa yeyote miongoni mwa wajumbe.

Amri na maelekezo.

6. Amri, maelekezo, notisi au nyaraka nyengine zilizofanywa au kutolewa kwa niaba ya Kamati zitasainiwa na:

(a) Mwenyekiti; au

(b) Katibu au mjumbe mwengine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kufanya hivyo kwa niaba ya Mwenyekiti.

Kamati inaweza kusimamia yenyewe mwenendo wa mikutano yake.

7. Kwa kuzingatia masharti ya Jadweli hili, Kamati inaweza kusimamia yenyewe mwenendo wa mikutano yake.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu za Mswada huu ni kuwezesha uendeshaji wa Mahakama na Tume ya Utumishi wa Mahakama kukuza uhuru wao katika kutoa huduma; kutokuegemea upande wowote na kuwajibika tu kwa mujibu wa masharti ya Katiba na sheria nyengine; kurahisisha utekelezaji wa taratibu za kimahakama zilizowekwa kwa ajili ya kutoa haki kwa wote; kurahisisha utaratibu wa kimahakama ambao unajifunga katika utoaji wa uamuzi kwa haraka; kurahisisha utaratibu wa kimahakama unajifunga katika usuluhishi wa migogoro; kuunga mkono na kuendeleza utaratibu wa kimahakama ambao unajifunga katika kuwalinda watu na haki zao; kukuza na kuendeleza taratibu za haki katika utekelezaji wa kazi na uendeshaji wa shughuli za Mahakama, na hususan, inaongozwa katika kesi zote ambazo Mahakama ina jukumu la kutoa maamuzi yanayowaathiri Majaji, Mahakimu na Makadhi wa ngazi yoyote au muajiriwa wake, kwa kutumia Kanuni za Haki za Msingi; kuwa ni muongozo wa usimamizi wa uhuru wa Mahakama na uwezo wa asili kulinda na kusimamia mwenendo wake yenyewe, kufikia malengo haya kwa njia ya kutumia misingi iliyowekwa katika Katiba na sheria nyengine na kuanzisha mfuko maalum wa Mahakama; na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Mahakama kwa Wazanzibari wote; na kutumia teknolojia ya kisasa katika uendeshaji wake.

Mswada unagawika katika Sehemu Saba:

Sehemu ya Kwanza inaweka masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina fupi na kuanza kutumika, matumizi, tafsiri ya maneno mbali mbali yaliyotumika katika Mswada huu na viwango vya utumishi.

Sehemu ya Pili inapendekeza masharti kuhusu utawala. Inaelezea masharti yanayohusu muundo wa utumishi wa Mahakama, uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, kazi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na watendaji wa Mahakama wasaidizi. Sehemu hii pia inaweka masharti kuhusu Tume ya Utumishi wa Mahakama, uwezo wa Tume, viapo, utaratibu na kinga. Pia, ina masharti ya kina kuhusu kazi za Tume. Pia inaweka masharti ya kufanya mapitio ya maslahi, kukasimu kazi, uwezo wa kuachisha kazi na kuondoa.

Sehemu ya Tatu inaweka masharti yanayohusiana na Jaji Mkuu na Mrajis. Inaainisha uwezo wa Jaji Mkuu na kazi za Mahakama. Inaweka masharti yanayohusu uteuzi wa Mrajis na kazi za Mrajis.

Sehemu ya Nne inatoa masharti kwa ajili ya uanzishaji wa Kamati za Maadili. Inaelezea muundo wa Kamati ya Maadili ya Majaji na Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama, kazi za Kamati hizo, malalamiko mbele ya Kamati hizo, aina na maudhui ya malalamiko. Pia, inaweka utaratibu wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama kushughulikia malalamiko.

Sehemu ya Tano ni kuhusu masharti ya fedha. Inaanzisha Mfuko wa Mahakama. Inaweka masharti kuhusu misaada, bajeti ya Mahakama, uwasilishaji wa makadirio ya bajeti katika Tume, majadiliano kuhusiana na makadirio ya bajeti na uwasilishaji.

Na pia Sehemu hii inajumuisha masharti kuhusu hesabu na ukaguzi na pia kuhusu usimamizi na udhibiti wa fedha za Mahakama.

Sehemu ya Sita ina masharti ya kina kuhusu makosa na adhabu. Sehemu hii inaweka makosa mbali mbali kama vile kosa la kushawishi au kujaribu kushawishi na kosa la kutoa taarifa za uongo kwa Tume. Sharti limewekwa katika Sehemu hii kwa ajili ya tafsiri ya neno "Tume". Sehemu hii pia ina masharti yanayokataza kuweka bayana taarifa zilizozuiliwa na ina masharti kuhusu idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Sehemu ya Saba inaweka masharti ya jumla kuhusu Kanuni na utekelezaji wa kazi chini ya Sheria hii. Sehemu hii pia inafuta baadhi ya vifungu katika Sheria ya Mahakama Kuu Nam. 2 ya 1985 na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011.

Mswada huu pia una Jadweli tatu.

HAROUN ALI SULEIMAN
Waziri, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,
Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Zanzibar

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - 2018